# SALAM KWA WAANDISHI WA HABARI MKOA WA RUKWA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI TAREHE 03 MEI, 2017

**Ndugu Mwenyekiti wa Rukwa Press Club,**

**Mlezi wa Press Club,**

**Wanachama wa Rukwa Press Club,**

**Wadau wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana.**

Ni jambo la kushukuru kwamba Mungu ametuwezesha kukutana katika ukumbi huu ikiwa ni maalum kuadhimisha siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari katika hali ya amani na salama. Napenda kuwashukuru kunialika niwe mgeni rasmi katika maadhimisho yenu haya kwa Mkoa wetu wa Rukwa. Napenda niwashukuru kwa uamuzi wenu na niseme asanteni kwa heshima hii mliyonipa.

Mkoa wa Rukwa kama mnavyofahamu ulianzishwa Mwaka 1974 baada ya sehemu ya Mkoa wa Tabora na Mbeya kumegwa na kuunganishwa. Ni Mkoa ambao una ukubwa wa Kilometa 27,765; kati ya hizo Kilometa 22,844 ni nchi kavu na Kilometa 4,921 ni eneo la maji. Tunazo Wilaya tatu zenye Halmashauri 4, Tarafa 16, Kata 97, Vijiji 354, Vitongoji 1,827, Mitaa 167 na Kaya 185,076.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Ni muhimu pia mkafahamu kwamba kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 Mkoa wa Rukwa ulikuwa na wakazi wapatao miliomi 104, 539; Wanawake wakiwa 517,228 na Wanaume 487,311. Mwaka huu tulionao wa 2017 Mkoa unakisiwa kuwa na wakazi wapatao 1,192,366 ambapo Wanawake ni 613,938 na Wanaume 578,428. Inakadiriwa vilevile kwamba idadi ya wanawake wenye uwezo wa kuzaa ni 265,477 na hivyo idadi ya watoto chini ya miaka 5 ni 238,473.

Kijiografia Mkoa wetu upo Kusini Mgharibi mwa Tanzania. Mkoa wetu unapakana na Katavi na Songwe. Zaidi ya hapo unapakana na Nchi ya Zambia upande wa Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo upande wa Magharibi. Nina sababu kubwa ya kuwaambia haya na ili muelewe mambo hayo na muweze kuona ni jinsi gani mtakavyoweza kutoa huduma kama waandishi wa habari katika Mkoa wa Rukwa.

Napenda niwapongeze kwamba Club yenu ilianzishwa Mwaka 2000 ikiwa na Wanachama 8 na kwamba club yenu sasa imepanuka na kuwa na wanachama 30 ambao kijinsia wanaume ni 22 na wanawake 8 ni jambo jema vilevile kwamba club ina usajili wa kudumu tangu mwaka 2003 baada ya kusajiliwa na Wizara Mambo ya Ndani. Ni dhahiri kwamba mpo mstari wa mbele kuzingatia na kufuata sheria.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa kazi mnayofanya katika Mkoa wa Rukwa ya kuwahabarisha wananchi kupitia vyombo mnavyovitumikia baadhi ikiwa ni redio, runinga na magazeti na sasa kwa Sheria mpya ya huduma za habari ni pamoja na mitandao ya kijamii. Kwa jiografia na hali halisi ya Mkoa wetu mpo wachache lakini mmekuwa mkifanya jitihada za kutoa habari mbalimbali.

Napenda kusema; kwa kipindi ambacho nimekuwa nanyi katika Mkoa huu tatizo la ushirikiano halipo. Jambo kubwa lililo mbele yetu ni kuendeleza na kudumisha ushirikiano huo kwa maslahi ya wananchi au wadau wa habari katika Mkoa wetu na taifa kwa ujumla.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Mmenifahamisha kwamba haya ni maadhimisho ya club za waandishi wa habari; maadhimisho ambayo yanafanyika mahsusi kwa kuadhimisha

siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari. Ninyi hapa mmeamua kufanya maadhimisho ya kimkoa hapa Sumbawanga. Naamini mtakuwa na mjadala ambao mtahitimisha kwa kupata mikakati mizuri zaidi katika kuendeleza tasnia ya habari.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Risala yenu pia imeonesha kwamba hampo peke yenu kwani nanyi ni wanachama wa club za Waandishi wa Habari Tanzania (UPTC) ambayo Makao yake Makuu yapo Mwanza ambayo imekuwa ikijenga uwezo wa vilabu vya Wanahabari kimafunzo na hata kuwapa vifaa vichache na vitendea kazi kama Camera, printers N.k.

Lakini vilevile nimefahamu kwamba RKPC ni mwanachama wa MCT ambapo pamoja na mambo mengine inasimamia maadili yenu mkiwa Waandishi wa habari. Naamini kadri mnavyojikita na kusaidia jamii kuamka kupitia habari mnazoandika hususani zile zinazolenga

maendeleo na kunyanyua kiwango cha maisha; jamii itaweza kuona umuhimu wa kazi yenu na kuwa tayari kuwaunga mkono kwa misaada mbalimbali. Nina shauku kubwa sana kuona hilo likitokea kwa ajili yenu.

Mkoa wetu ni wa Kilimo cha mazao ya chakula, biashara, ufugaji, uvuvi, utalii na madini. Shughuli ambazo zinahitaji msukumo wa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na ninyi waandishi wa habari kusemea kwa nguvu maeneo hayo.

Mnayo nafasi kubwa ya kutangaza fursa zilizopo katika mkoa wetu wa Rukwa na watu wengine walio nje waweze kujua fursa hizo na kuja kuungana na wananchi wa Mkoa huu kuwekeza katika sekta nilizozitaja na hasa viwanda ambavyo vinaweza kusaidia kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa ili kukamata masoko yaliyo ndani, nje ya Mkoa na nchi jirani.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Mwandishi wa Habari ni nani?

Ni mtu aliyesajiliwa kama Mwandishi wa Habari chini ya Sheria No. 12 ya Mwaka 2016 iliyopitishwa na Bunge letu na tarehe 16 Novemba, 2016 ikaidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mwandishi huyu anayetajwa na sheria ndiye ambaye anakusanya, anahariri, anaandaa na kutangaza makala na taarifa na awe ameajiriwa na chombo cha habari au Mwandishi huru. Hii ina maana kwamba mtu hataruhusiwa kufanya kazi za habari isipokuwa kama amethibitishwa kwa mujibu wa Sheria. Naamini kwamba sasa mna uhakika kwamba sheria inalinda tasnia yenu ya habari.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Kauli mbiu yenu ya mwaka huu: “Club za waandishi wa habari zina wajibu wa kuendeleza amani katika jamii”. Napenda niungane nanyi kwa kauli mbiu hii ambayo inaendana na sifa ya

nchi yetu kwamba ni ya amani. Mnao wajibu wa kulinda na kutetea amani hiyo kwa kutumia vyema tasnia yenu ya habari ambayo ikitumika vibaya ni rahisi sana kuvuruga umoja, mshikamano na muungano wa Taifa letu tena kwa sekunde chache. Amani inapovunjika haitabagua nani mwandishi na nani siyo mwandishi. Itaathiri kila mtu na kila kitu.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imepania kupambana na vitendo viovu ikiwepo la madawa ya kulevya, ujangili, uharibifu wa mazingira, ukwepaji wa kulipa ushuru, ufisadi. Tasnia ya habari katika mapambano hayo ina jukumu kubwa ili kuepusha madhara yatokanayo na mambo hayo.

Napenda nitoe rai kwenu kwamba itapendeza kalamu zenu na visemeo vyenu mkaelekeza katika kuunga mkono juhudi hizo mkielimisha jamii bila

ya kuchoka, kukata tamaa au kurubuniwa kwa namna yoyote ile na wale wasioitakia nchi yetu mema.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Ninyi mkiwa waandishi wa habari na wengine tukiwa wadau tunafahamu kwamba mnaadhimisha siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari. Jambo kubwa ambalo ningependa kusisitiza kwenu ni lile la kujua kwamba hakuna uhuru usiokuwa na mipaka na wala hakuna haki isiyokuwa na wajibu. Katika hili mna nafasi kubwa ya kufanya kazi yenu kwa misingi ya sheria zinazotawala tasnia ya habari na hasa mkizingatia tunayo sheria mpya Namba 12 ya mwaka 2016 ya huduma za habari. Nawaomba sana muisome sheria hii na kuielewa badala ya kutanguliza hofu; sheria inatamka bayana; kutakuwepo na baraza litakalojulikana baraza huru la habari. Katika baraza hilo miongoni mwa wajumbe watakuwa ni waandishi wa habari tena wazoefu katika masuala ya habari. Naamini mambo mengi katika sheria hiyo yanaendelea

kufanyiwa kazi na yakikamilika yatawafikia na hata sisi wadau.

Nawatakia maadhimisho mema na natoa ahadi ya kutoa ushirikiano kwenu na wale wote ambao wapo katika Halmashauri. Ni jambo jema kwamba Serikali sasa ina Maafisa Habari kwenye ngazi hizo. Niwatake na wadau wengine waendelee kutoa ushirikiano kwa klabu ya Waandishi wa Habari Rukwa.

***Mwenyekiti wa Club ya Waandishi wa Habari,***

Nataka niwaombe tunapowahitaji ninyi muwe wepesi, lakini pia nitoe agizo sitaki kusikia Halmashauri za Mkoa wa Rukwa wanakwepa kutoa habari. Ni vyema sasa Halmashauri zione umuhimu wa kuwatumia wanahabari kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unaongezeka na nisisitize uwepo uwazi kwa shughuli zote za maendeleo katika Halmashauri zote.

Napenda nisisitize kwamba mnapoandika habari mkumbuke kuweka mbele umoja wa Taifa letu, usalama wetu, uhuru wa nchi, uadilifu na maadili ya jamii kwa upande mwingine.

**Zelote Stephen Zelote**

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**